# NIMEKUTANA NA YESU

**“Pingu za yaliyopita zimeniondoka”**

**Andiko Kuu: Yohana 4:1–30**

(Mwanamke Msamaria)

---

## UTANGULIZI

Kuna magereza mabaya sana duniani,
lakini si yote yamejengwa kwa vyuma.

Gereza baya zaidi ni gereza la mawazo.

Watu wengi wako hai kimwili,
lakini wamefungwa:

- Kiakili
- Kihisia
- Kiroho

Wengine ni wafungwa wa:

- Zamani yao
- Makosa yao
- Kushindwa kwao
- Familia zao
- Eneo walilotoka
- Elimu yao
- Maneno yaliyosemwa dhidi yao

Wameishi maisha yao wakibeba lebo:

- “Huwezi kufanikiwa.”

- “Hakuna kitu kizuri kinaweza kutoka kwenu.”
- “Watu wa eneo lenu hawaendi mbali.”
- “Umeharibu maisha yako.”
- “Wewe hufai.”

Na kadiri muda unavyopita,
wanaanza kuamini hayo maneno.

Lakini leo Mungu amenituma nikutangazie:

**Usiwe mfungwa wa zamani yako.**

Wewe si makosa yako.
Wewe si mazingira yako.
Wewe si maneno ya watu.
Wewe si kile shetani anasema kuhusu wewe.

**Wewe ni kile Mungu amesema wewe ni.**

Mwanamke Msamaria alikuwa:

- Ameumizwa
- Amevunjika moyo
- Amehukumiwa
- Amekataliwa
- Ana historia mbaya

Lakini kukutana kwake na Yesu kulibadilisha maisha yake kabisa.

Na leo natangaza:

**Zamani yako haitaharibu hatima yako.**

---

**MFANO**

Mtu mmoja alichukua noti ya pesa iliyokuwa:

- Imechakaa
- Imefinyangwa
- Imeangushwa chini
- Imejaa uchafu

Akauliza watu:
“Hii ina thamani gani?”

Wakasema:
“Bado ni pesa kamili.”

Akaikanyaga tena.
Akaikunja tena.

Kisha akauliza:
“Sasa ina thamani gani?”

Wakasema:
“Bado ina thamani ile ile.”

Kwa nini?

Kwa sababu thamani yake haikubadilika kutokana na ilichopitia.

Sikiliza vizuri:

Unaweza kuwa:

- Ulikataliwa
- Ulidharauliwa
- Ulisemwa vibaya
- Ulivunjwa moyo
- Ulipitia maumivu

Lakini mbele za Mungu,
thamani yako haijawahi kupungua.

Watu wanaweza kuona uchafu,
lakini Mungu anaona hatima.

## Hebu fikilia

Mwanamke Msamaria alikuja kisimani mchana wakati jua limewaka vizuli, sio kawaida, kwa kawaida watu huchota maji asubuhi au jioni hana ukikubuka yale ni maeneo ya jua kali wakati jua sio kali, tena wamama hupeda kueneda wakiwa anga wawili, lakini huyu:

Peke yake, jua ndili hilo, kwa sababu…
kwa sababu alikuwa anaepuka watu.

Labda alisema:
"Nikienda asubuhi wale wamama wataanza tena kikao cha kunijadili!"

Kuna watu wanajua habari zako kuliko wanavyojua mistari ya Biblia!

Lakini tunamshukuru Mungu,
Yesu hakwenda Samaria kumhukumu.

Alienda kumwokoa.

Usihovu,Yesu anajua historia yako lakini hiyo haijabandisha mtazamo wake kwako.

**"Yesu anajua historia yangu lakini bado ananipenda!"**

---

## 1. YESU ATAKUKUTA ULIPO

**Yohana 4:6-7**

“Yesu akaketi kisimani…”

Yesu alimkuta:

- Katika Samaria
- Katika maumivu
- Katika aibu
- Katika upweke

Hakuwa kanisani.
Hakuwa akiomba.
Lakini Yesu bado alimtafuta.

Hiyo ndiyo neema.

Haijalishi uko hali gani leo,
Yesu bado anaweza kukufikia.

---

## 2. Usifungwe nira ya mahali ulipotoka, kata pingu

Msamaria alikuwa anatoka eneo lililodharauliwa.

Wayahudi waliidharau Samaria.

Na hata leo,
watu wanaweza kukudharau kwa sababu ya:

- Kijiji chako
- Familia yako
- Mazingira yako
- Hali yako ya maisha

Lakini sikiliza:

**Mungu hafungwi na jiografia.**

Daudi alitoka malishoni.
Yusufu alitoka gerezani.
Yesu alitoka Nazareti.

**Yohana 1:46**

“Kuna jambo jema laweza kutoka Nazareti?”

Lakini Mwokozi alitoka huko.

Mahali ulipotoka
hapawezi kuzima hatima yako.

Hatima yako imefungwa kwa Mungu,
si kwa mazingira yako.

---

## 3. USIWE MFUNGWA WA ZAMANI YAKO

**Yohana 4:18**

“Umekuwa na waume watano…”

Yesu alijua historia yake yote.

Alijua:

- Makosa yake
- Maumivu yake
- Kushindwa kwake

Lakini bado alimpenda.

Shetani anataka:

- Uishi kwa lawama
- Uishi kwa aibu
- Uishi kwa kujihukumu

Anakuambia:

- “Umeshindwa.”
- “Mungu hawezi kukutumia.”
- “Maisha yako yameharibika.”

Lakini shetani ni mwongo.

**Shetani anaweza kujua historia yako,**

lakini hajui kesho yako.

**Yeremia 29:11**

“Mawazo ninayowawazia ni ya amani… niwape tumaini na mwisho mwema.”

Maisha yako hayajaisha.
Bado una kesho.
Bado una kusudi.

---

## 4. WEWE SI MANENO YA WATU

Watu wanaweza:

- Kukuhukumu
- Kukudharau
- Kukusema vibaya
- Kukutazama kwa macho ya zamani

Huenda mwanamke huyu alikuwa gumzo mjini.

Lakini Yesu hakufuata maoni ya watu.

Sikiliza vizuri:

**Usijenge utambulisho wako juu ya maoni ya watu.**

Watu wanaweza kujua makosa yako,
lakini hawajui mpango wa Mungu juu ya maisha yako.

Wale waliomcheka Yusufu,
baadaye walimsujudia.

Wale waliomdharau Daudi,
baadaye walimshangilia.

Na wale wanaokudharau leo,
wanaweza kushangaa kesho Mungu atakapokuinua.

---

## 5. UMEUMBWA KWA NJIA YA AJABU

### Zaburi 139:14

“Nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu na ya kutisha.”

Wewe si ajali.
Wewe si wa kawaida.
Wewe si bure.

Mungu alikuumba kwa kusudi.

Ndani yako kuna:

- Uwezo
- Wito

- Hatima
- Kesho kubwa

Shetani anakupiga vita
kwa sababu anaogopa kile utakachokuwa.

---

## 6. HATIMA YAKO IKO MIKONONI MWA MUNGU

Hatima yako haiko:

- Kwa watu
- Kwa shetani
- Kwa mazingira
- Kwa historia yako

**Hatima yako iko mikononi mwa Mungu Mwenyezi.**

**Isaya 46:10**

“Shauri langu litasimama…”

Mungu akisema:
“Utainuka,”
hakuna shetani atakayekuzuia.

Mungu akisema:
“Utafanikiwa,”
hakuna historia itakayokufunga.

Mungu akisema:
“Una kesho,”
hakuna mwanadamu atakayebadilisha hilo.

## 7. KUKUTANA NA YESU HUBADILISHA KILA KITU

### Yohana 4:28

“Yule mwanamke akaiacha gudulia yake…”

Aliacha:

- Aibu
- Hofu
- Lawama
- Utambulisho wa zamani

Na akawa shahidi wa Kristo.

Mtu mmoja aliyekuwa akijificha,
akawa mhubiri wa mji mzima.

Kukutana na Yesu hubadilisha:

- Mawazo yako
- Mwelekeo wako
- Kesho yako
- Maisha yako

---

## HITIMISHO

Mwanamke Msamaria aligundua kuwa:

Hakufafanuliwa tena na: (she was no longer defined)

- Samaria
- Zamani yake
- Kushindwa kwake
- Maneno ya watu

- Historia yake

Alifafanuliwa na kukutana kwake na Yesu. (she was now defined by her encounter with Jesus)

Na leo,
Mungu anabadilisha hadithi ya mtu.

Wewe si:

- Kile watu wanasema
- Kile shetani anasema
- Kile historia yako inasema

Wewe ni:

- Mteule wa Mungu
- Uliyekombolewa
- Uliyeumbwa kwa ajabu
- Uliyeitwa kwa kusudi
- Mwenye hatima kubwa

Zamani yako iko nyuma yako.

Kesho yako iko mbele yako.

Na hatima yako iko mikononi mwa Mungu Mwenyezi.

**TAMKO YA IMANI**

- Nimekutana na Yesu!
- Mimi si mfungwa wa zamani yangu!
- Sifafanuliwi na makosa yangu!
- Sifungwi na mazingira yangu!
- Mimi si maneno ya watu!
- Mimi si maneno ya shetani!
- Nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu!

- Nina kesho njema!
- Nina hatima kubwa!
- Mungu ana mpango juu ya maisha yangu!
- Zamani yangu haitazika kusudi langu!
- Hatima yangu iko mikononi mwa Mungu!
- Nitainuka tena!
- Nitashinda!
- Aibu imeondoka!
- Kesho yangu ni kubwa kuliko jana yangu!
- Nitafanikisha kusudi la Mungu!

Pasa sauti kwa Imani utangaze:

**“NIMEKUTANA NA YESU!”**